

## TEZI DUME NI NINI?

- ❖ Tezi dume ni moja ya tezi la uzazi la kiume ambalo kila mwanaume analo, tezi hili lipo chini ya kibofu cha mkojo na linazunguka njia ya mkojo toka kwenye kibofu kwenda kwenye uume.
- ❖ Jinsi umri unavyoongezeka tezi dume nalo huongezeka ukubwa ambaou unaweza kuwa wa kawaida au saratani.
- ❖ Kuna aina tatu za magonjwa ya tezi dume.
  - Maambukizi ya Bakteria (Prostatitis).
  - Kukua kwa tezi dume ambalo sio saratani (Benign Prostatic Hypertrophy-BPH).
  - Saratani ya tezi dume.

## KAZI YA TEZI DUME

- ❖ Kutoa majimaji anayochanganyika na mbegu za kiume (sperms) kutengeneza manii (semen).

## SARATANI YA TEZI DUME

- ❖ Saratani ya tezi dume inashika nafasi ya tatu kwa kusababisha vifo vitokanavyo na saratani kwa wanaume duniani.
- ❖ Pia ni chanzo kikuu cha vifo vinavyosababishwa na saratani kwa wanaume wenye umri wa miaka 70 na kuendelea.

## VITU VINAVYOSABABISHA SARATANI YA TEZI DUME

- ❖ Chanzo hasa cha saratani ya tezi dume hakijulikani, saratani hii ina uhusiano mkubwa na;
  - Umri,Wanaumewenyeumrikuanzia miaka 60 na kuendelea wanapata zaidi saratani ya tezi dume.
  - Vyakula vyenye kiasi kikubwa cha mafuta, hasa ya wanyama.
  - Historia ya tatizo hili kwenye familia (Genetic).
  - Kuwa na uzito uliokithiri.

## DALILI ZA SARATANI YA TEZI DUME

- ❖ Katika hatua za awali, dalili hazitofautiani sana na zile za kuvimba kwa tezi dume lisilokuwa saratani (BPH). Dalili hizo ni pamoja na;
  - Kusikia kupata haja ndogo mara kwa mara hasa nyakati za usiku
  - Haja ndogo kuchelewa kutoka unapoanza kukojoa.
  - Kutoa mkojo wenye mtiririko dhaifu na kuchuruzika kidogo kidogo baada ya kumaliza kukojoa.
  - Kujikakamua wakati wa kukojoa na kushindwa kumaliza mkojo wote.
  - Kutoa mkojo au manii yaliyochanganyika na damu
  - Maumivu makali sehemu mbalimbali za mwili kama saratani imesambaa.
  - Kupungauzito,kuhisikichefuchefu, uchovu na kizunguzungu.

## UCHUNGUZI / UPIMAJI

- ❖ Uchunguzi kwa kutumia kidole cha shahada kupidia njia ya haja kubwa na kuhisi ukubwa wa tezi kwenye ukuta wa puru.
- ❖ Kipimo cha damu kuangalia kiwango cha aina ya 'protein' iitwayo 'Prostate Specific Antigen (PSA)', proten' hii huwa juu kuliko kawaida kama mtu ana saratani ya tezi dume na wakati mwingine kama ana maambukizi (prostatitis).
- ❖ Kuchukua kipande cha nyama kwenye tezi (Prostate Biopsy) kwa uchunguzi wa kimaabara.
- ❖ Kipimo cha mawimbi sauti (Ultrasound) ambacho husaidia kuonyesha ukubwa na sura ya tezi dume.
- ❖ Vipimo vya CT scan, MRI kutambua kama saratani imesambaa sehemu nyingine za mwili.

## TIBA YA SARATANI YA TEZI DUME

- ❖ Matibabu ya saratani ya tezi dume

yanategemea hatua ya ugonjwa na umri wa mgonjwa.

- ❖ Aina za tiba hizo ni pamoja na;
  - Upasuaji (Surgey)
  - Mionzi (Radiotherapy)
  - Vichochezi (Homonal therapy)
  - Kemikali (Chemotherapy)-
  - Ubaridi (Cryotherapy)

## KINGA

- ❖ Fanya mazoezi ya mwili na uwe na uzito unaostahili ukilinganisha na urefu wako.
- ❖ Kula vyakula vyenye mafuta kiasi na hasa ya mimea, vyakula vyenye asili/ vyenye soya, vyakula vyenye "Lycopene" – inapatikana kwenye nyanya, tikiti maji, na matunda mengine, mboga za majani kwa wingi na samaki.

### Kwa maelezo zaidi wasiliana na:

Kituo cha Afya-Chuo Kikuu cha DSM  
Simu: 2410500-8 Ext. 2006  
: 2410014


Barua pepe: [healthcentre@udsm.ac.tz](mailto:healthcentre@udsm.ac.tz)



## CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM

## KITUO CHA AFYA

S.L.P. 35074  
DAR ES SALAAM



# SARATANI YA TEZI DUME

'A Healthy Mind Thrives in a Healthy Body'